

HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE WAKATI WA
UZINDUZI WA SACCOS YA UWT PEMBA
MKOA WA KUSINI PEMBA - TAREHE 13 MEI, 2010

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba,

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa Kusini Pemba

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kusini Pemba

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kusini Pemba

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya

Mwenyekiti wa SACCOS ya UWT Pemba

Makatibu wa UWT Pemba

Viongozi wote wa Chama na Serikali

Wanachama wote wa SACCOS

Wageni waalikwa

Mabibi na Mabwana

Aslaam Aleykhum!

Naomba mniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo. Aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wote kwa ujumla kwa mapokezi mazuri, tangu nimewasili hapa Pemba.

Pia nichukue fursa hii kuwapeni ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete, anawasalimu sana!

Viongozi, mabibi na mabwana

Kabla ya kuanza, ningependa nieleze lengo la kufika kwangu hapa leo. Nimefika hapa kwa ajili ya kuhamasisha shughuli za Maendeleo kupitia mikutano ambayo inanipa fursa ya kuzungumza nanyi.

Hata hivyo, nipo hapa kwa ajili ya kuzindua SACCOS ambalo ni jambo muhimu sana. Pia nitumie fursa hii kuwapongeza wana SACCOS wote na wana UWT kwa kuweza kufanikisha mkutano huu. Aidha, niwapongeze wale wote waliotoa wazo la kuanzisha SACCOS hii. Kwani kuanzisha SACCOS ni njia moja ya kutekeleza ilani ya uchaguzi, inayotaka kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa ili kumuwezesha mwananchi.

Hivyo, muitumie vizuri fursa hii kwa kuweka akiba zenu kwa matumizi ya baadae, lakini pia kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Ndugu wananchi

Nina fahamu kuwa wanawake tuna majukumu mengi ya kifamilia, ambayo yanatufanya tushindwe kushiriki vizuri katika shughuli mbali mbali za Maendeleo.

Lakini naomba nitoe wito kwenu, majukumu haya yasiwe kikwazo cha kushiriki katika shughuli za Maendeleo. Kwani nafahamu kuwa mbali na majukumu hayo lakini pia tunakabiliwa na changamoto nyingi ambazo ni vikwazo katika jitihada za kujiendeleza. Inawezekana kabisa ni kutokana na mfumo uliopo na mila na desturi zetu ambazo zinamfanya mwanamke akose fursa mbalimbali kama elimu inayoweza kuwapa ufahamu wa kutambua umuhimu wa SACCOS. Lakini wakati mwingine ni sisi wanawake tunajirudisha nyuma.

Ndugu wananchi

Kwa kutambua hilo mimi kama mwanamke, na mama wa Taifa hili niliamua kuanzisha taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) ili niweze kutoa fursa kwa wanawake katika Elimu, Afya na Uchumi.

Leo tumekusanyika hapa kwa ajili ya uzinduzi wa SACCOS, jambo ambalo ni muhimu sana katika kumsaidia mwanamke ili aweze kujikwamua kiuchumi. Pia niwaase wanawake wenzangu juu ya ushirikiano katika shughuli zote za Maendeleo. Kwani kwa kufanya hivyo, mtafanikiwa sana kwani **umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu**. Na umoja huwa na nguvu zaidi ikiwa mtakuwa wengi. Hivyo, ni jukumu letu kuongeza wanachama wa SACCOS na wanachama wa UWT pia.

Viongozi, Mabibi na Mabwana

Suala la kurejesha mikopo kwa wanachama wa SACCOS ni la muhimu sana. Kwani tunaporejesha mikopo kwa wakati, itatusaidia kutoa nafasi kwa wanachama wengine kukopa na hivyo wanachama wote kupata manufaa ya SACCOS yaliyokusudiwa.

Viongozi, Mabibi na Mabwana

Kwa upande wa UWT napenda kuwakumbusha wanawake kuwa, nguvu ya chama ni wingi wa wanachama walio hai.

Yaani wanachama ambao wanalipa ada zao kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa. Nimetaarifiwa kuwa ulipaji wa ada bado sio mzuri. Nawashauri wanachama mjitahidi kulipa ada zenu ili kuupa nguvu umoja wetu. Ningependa pia kusisitiza tena kuimarisha ushirikiano na upendo.

Tuwape moyo na kuwasaidia viongozi wanawake waliopo madarakani na wale ambao wanagombea nafasi mbalimbali. Kwani hao ndio wawakilishi wetu watakao tetea mambo yanayowagusa wanawake.

Ndugu wananchi

Nimefurahishwa sana na taarifa kuwa hapa pemba kuna vikundi mbali mbali vya ujasiriamali zikiwemo shughuli za Upandaji miti, Ususi wa mikeka, Ufumaji na uvuvi. Hii ni hatua nzuri ya Maendeleo, ***Hongereni sana.***

Baada ya kusema hayo nichukue fursa hii kutamka kuwa, **“SACCOS HII YA IMEZINDULIWA RASMI LEO TAREHE 13 /05/2010”.**

Ahsanteni kwa kunisikiliza Mungu Awabariki!